

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO  
SHULE YA SEKONDARI NDURUMO  
S.L.P 383 LUSHOTO  
SIMU: 0621-403510 au 0769-003985 au 0620-151265

15/12/2020

**Kumb. Na. NDUSS/JI/VOL.I/2021/1**

NDUGU .....  
.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI NDURUMO

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujunga na KIDATO CHA KWANZA kwa mwaka wa masomo wa 2021 katika shule ya sekondari NDURUMO iliyoko Kata ya Rangwi, Tarafa ya Mtae, Mkoa wa Tanga.

Umechaguliwa kutokana na kufaulu vizuri mitihani yako ya darasa la saba mwaka 2020. Hivyo ukiwa Ndurumo Sekondari unatakiwa kusoma kwa bidii na maarifa ili uitumie nafasi hii uliopewa na jamii, na serikali vizuri kwa manufaa yako binafsi, manufaa ya jamii nzima na Taifa kwa ujumla.

Ukiwa Ndurumo Sekondari utalazimika kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu pamoja na maadili ya kiuanafunzi (Sheria za shule zimeambatanishwa katika kiambatisho C). Ukienda kinyume na sheria hizi utafukuzwa shule kwani utovu wa nidhamu hautavumiliwa.

Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe 11/01/2021 siku ya Jumatatu saa 2.00 kamili asubuhi ukiwa na mzazi wako kwaajili ya maelekezo na maandalizi. Masomo yataanza rasmi tarehe 18/01/2021 siku ya Jumatatu kuanzia saa 1.15 asubuhi.

Utajaza viambatisho vifuatavyo na kuleta shuleni.

**Kiambatisho A:** Fomu ya kuandikishwa shuleni na taarifa muhimu za mwanafunzi na mzazi/mlezi.

**Kiambatisho B:** Fomu ya kujua afya ya mwanafunzi (Medical Examination Form). Fomu hii ijazwe na daktari wa hospitali au zahanati ya serikali.

**Kiambatisho C:** Ni sheria za shule. Unapaswa kuzisoma na kuzielewa.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

- (i) Fika shuleni ukiwa na cheti cha kuzaliwa. Kama hauna nenda mahakamani ili uape upewe Hati (Affidavit) ili kuthibitisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania.
- (ii) Fika na viambatisho vya fomu A, B na C zikiwa zimejazwa kikamilifu na wahusika wote.

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

**(1) SARE ZA SHULE (Wasichana)**

- (i) Mashati mawili (2) **meupe** ya mikono mifupi aina ya TOMATO

Kwa Waislamu awe na nusu kanzu mikono mirefu pamoja na Hijab nyeupe aina ya **Halua halua**

- (ii) Masweta mawili rangi ya **maroon (damu ya mzee)** shingo ya V (Yatapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/- tu)

(iii) Sketi mbili (2) za heshima, ndefu hadi chini ya magoti rangi ya **kijani iliyokolea (Dark Gree)**

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi pea 2 vya kufunga na kamba (visiwe vya buti au vyenye visigino virefu) pamoja na soksi nyeupe.

(v) Kwa kuwa maeneo haya ni ya mvua anatakiwa awe na Buti kwaajili ya nyakati za mvua na matope.

**2. SARE ZA SHULE (Wavulana)**

- (i) Suruali mbili (2) za heshima rangi ya **Kijani iliyokolea (Dark Gree)**

(ii) Mashati mawili (2) MEUPE yenyé mikono mifupi aina ya TOMATO

(iii) Masweta mawili rangi ya **maroon au damu ya mzee** shingo ya V (Yatapatikana shuleni kwa sh. 15,000/- tu).

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi pea 2 vya kufunga na kamba (visiwe vya buti au vyenye visigino virefu) pamoja na soksi nyeusi.

(v) Mkanda mweusi wa ngozi wa suruali wenye "buckle" ndogo.

(vi) Kwakuwa maeneo haya ni ya mvua anatakiwa awe na buti kwaajili ya nyakati za mvua na matope

### **3. NGUO ZA MICHEZO**

Anatakiwa awe na Nguo za michezo ambazo ni:

- (i) Bukta rangi ya **blue**.
- (ii) Fulana (T-shirt) rangi ya **maroon (damu ya mzee)** yenyenembo ya shule (inapatikana shuleni kwa sh. 10,000/- tu ).
- (iii) Raba za michezo jozi moja (01)
- (iii) Kwa wasichana awe na sketi fupi rangi ya **maroon (damu ya mzee)** iliyoshonwa mtindo wa solo

### **4. MAHITAJI YA DARASANI**

Kwa upande wa masomo anatakiwa aje na mahitaji yafuatayo;

- (i) Daftari kubwa (counter books) 3 QUIRE zisizopungua 12 pamoja na kalamu za bluu au nyeusi.
- (ii) Mathematical set (Mkebe wa vifaa vya Mahesabu) moja.
- (iii) Karatasi za grafu (graph pad) kwa ajili ya somo la Hisabati
- (iv) Faili mbili (02) za plastiki kwaajili ya kutunzia taarifa zake
- (v) Picha mbili (Passport size)
- (vii) Kamusi moja ya kiingereza (Dictionary) kwa matumizi yake ya kujifunzia lugha ya kiingereza.
- (viii) Begi la mgongoni la kubebia madaftari vitabu na vifaa vingine vya shule

### **5. ZANA ZA KAZI**

Aje na na ndoo ndogo ya lita 10 na jembe moja pamoja na mpini.

### **6. MICHANGO MINGINE**

Licha ya debe moja la mahindi na kilo 5 ya maharae Michango iliyopitishwa na wazazi kwa mwaka ni ile inayohusiana na chakula cha mchana, mwalimu wa sayansi..

1	Mwalimu wa sayansi kwa mwaka	12,000
2	Mlinzi	6,000
3	Wapishi na mafuta	20,000
	Jumla yote kwa mwaka	38,000

Kuna kamati maalum za wazazi kwaajili ya kushughulikia chakula na michango mbalimbali shuleni (**Kiambatisho E**).

Wafahamu wanakamati walioteuliwa na wazazi tarehe 03/10/2019 kwaajili ya kufuatilia chakula cha wanafunzi na mchango ya mlinzi na mwalimu wa sayansi.

NA.	KIJIJI	JINA LA MWANAKAMATI	NAMBA ZA SIMU
1	NKELEI	Mtendaji wa Kijiji cha Nkelei	
		Mama neema	0624-842103
		Zakati hamidu	0623-066870
2	KIRANGA	Mtendaji wa kijiji cha Kiranga	0624-933552
		ombeni emmanuel	0622-601143
		Elibariki Joseph	0622-565768
3	GOKA	Mtendaji wa kijiji cha Goka	0620-133583
		Joyce Madeghe	0629-165462
		Hammadi shabani (mlinzi wa shule)	0789-282193

### **7. HITIMISHO**

Utakapofika hapa shuleni utasomewa tena sheria za shule na utaratibu mzima wa shule hii na utalazimika kuufuata. Ukitifanya makosa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.

Endapo mwanafunzi atakuwa na dharura, mzazi/mlezi awasiliane kwa kutumia simu zilizotajwa hapo juu.

Mwishes natumia fursa hii kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shuleni na naamini utatumia vizuri nafasi hii uliyopewa na Taifa ya kukuongezea elimu yako.

KARIBU SANA.

.....  
Massawe I.M

MKUU WA SHULE

**KIAMBATISHO A:**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO  
SHULE YA SEKONDARI NDURUMO  
S.L.P 383 LUSHOTO  
SIMU: 0621-403510 au 0769-003985 au 0620-151265

15/12/2020

**Kumb. Na. NDUSS/JI/VOL.I/2021/2**

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA WAZAZI WA MWANAFUNZI

SEHEMU A: (HABARI ZA MWANAFUNZI): IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. Majina yako kamili (Kama kwenye mtihani) wa darsa la saba .....  
.....
2. Tarehe ya kuzaliwa ..... Dini.
3. Mahali na Wilaya ulipozaliwa .....  
.....
4. Shule ulipomaliza darasa la saba.....
5. Kidato unachokuja kuingia hapa shule ya Sekondari ya NDURUMO .....
6. Namba yako ya mtihani wa darasa la saba ilikuwa .....

**7. MICHEZO UNA YOPENDA**

NA.	AINA YA MCHEZO
1	
2	
3	

8. Kazi yeote uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k.  
.....

**9. MADARAKA/UONGOZI ULIOWAHI KUFANYA UKIWA SHULENI**

Na.	Madaraka/uongozi	Shule	Mwaka
1			
2			
3			

10. Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo (kama vile michezo, mpira, bustani, ushonaji viatu, nguo, michezo ya kuigiza, kuimba n.k)  
1..... 2 ..... 3 .....
11. Ndugu wa karibu wanaokulea (wa kiume/wa kike) k.m. Mjomba, mama, shangazi, babu, bibi kaka, dada , n.k .

Na	MAJINA KAMILI YA NDUGU	UHUSIANO	ANAKOISHI	NAMBA ZA SIMU
1				
2				
3				
4				

**Uthibitisho:** Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kweli. Naahidi kuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe: ..... Sahihi ya Mwanafunzi .....

#### SEHEMU B: (HABARI ZA MZAZI/MLEZI): IJAZWE NA MZAZI

1. Jina kamili.....
2. Kazi yake.....
3. Mahali anapoishi (Kitongoji) .....
- Kijiji..... Kata .....
4. Namba za simu.....

**Uthibitisho:** Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni za kweli. Naahidi kushirikiana na walimu kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe ..... Sahihi ya Mzazi/Mlezi .....

**KIAMBATISHO B:**

PMO-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO

NDURUMO SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL EXAMINATION FORM

From the Headmaster,  
NDURUMO Secondary School,  
P.O. BOX 383,  
LUSHOTO.

Date: .....

**Kumb. Na. NDUSS/JI/VOL.I/2021/3**

The Medical Officer .....  
(GOVERNMENT M.O)

Name of Student .....

**RE: SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

I shall be very grateful if you will kindly examine the above named student and give us a report regarding his fitness to undertake studies well in our school.

**A. PRELIMINARY INFORMATION: MEDICAL HISTORY (Tick the appropriate one)**

S.N	DISEASE	YES	NO	S.N	DISEASE	YES	NO
1	Tuberculosis			8	Skin Disorder /Disease		
2	Asthma			9	Anaemia		
3	Pneumonia			10	Eye problem / disorder		
4	Hart trouble			11	V.D		
5	Kidney trouble			12	Disabled		
6	Nervous breakdown			13	Operation		
7	Ear / nose / throat			14	Jaundice		

**B. VITAL STATISTICS**

Age ..... Height ..... Weight ..... Blood group ..... Blood pressure ..... Pulse rate .....  
Systolic ..... Diastolic .....

**C. MEDICAL EXAMINATIONS**

Examine this pupil in these area(s) and any area (s) deemed fit or unfit please. Delete whichever not applicable and provide recommendation (s) where necessary.

- (i) EARS: **RT Ear:** Yes/No..... **LT Ear:** Yes/No.....
- (ii) EYES: **RT Eye:** Yes/No..... **LT Eye:** Yes/No.....
- (iii) VISION: **Low:** Yes/No..... **High** Yes/No..... **Normal:** Yes/No .....

- (iv) ABDOMINAL EXAMINATION: **Liver:** Yes/No ..... **Spleen:** Yes/No .....
- (v) THROAT: Yes/No .....
- (vi) CHEST EXAMINATION: Yes/No.....
- (vii) M.S. SYSTEM: **Upper Limbs:** Ye/No..... **Lower Limbs:** Yes/No .....
- (viii) Any other physical impairment: Yes/No (State) .....

#### D. LABORATORY EXAMINATION

Please examine this pupil in these area(s) and any area (s) related to the laboratory investigation and give recommendations where necessary.

- (i) STOOL: **Ova** ..... **Leucocytes** .....
- (ii) URINALYSIS: **Protein:** ..... **Glucose** .....
- (iii) SEDIMENT: **Ova** ..... **Leucocytes** .....
- (iv) BLOOD: **Hb** ..... **B/S** ..... **VDRL** .....
- (v) Any blood investigation .....

#### E. MEDICAL CERTIFICATE:

We request the medical officer to complete the following:

I have examined the above named student and considered that he/she is physically fit/unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above. I recommend therefore the student to pursue/not to pursue studies to this school because .....

.....  
.....  
.....

Thank you in advance.

Dr's Name: ..... Signature ..... Date .....

Designation ..... Official stump .....

## KIAMBATISHO D:

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO  
SHULE YA SEKONDARI NDURUMO  
S.L.P 383 LUSHOTO  
SIMU: 0621-403510 au 0769-003985 au 0620-151265

15/12/2020

### Kumb. Na. NDUSS/JI/VOL.I/2021/4

#### SHERIA, TARATIBU NA KANUNI (STK) ZA SHULE

Shule ya sekondari NDURUMO inaongozwa kwa kufuata Katiba ya nchi, Sera ya Elimu, Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake pamoja na nyaraka na miongozo ya Kisera inayotolewa na Kamishna wa Elimu na miongozo ya kiutekelezaji inayotolewa na mamlaka nyingine zinazohusika.

#### 1. SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

(i) **Nidhamu na Heshima:** Hii ni pamoja na kutoa heshima kwa walimu, wakubwa na wageni kwa kusalimia ukiwa umesimama na kuwapokea walimu, wageni na wakubwa mizigo waliyobeba.

Mavazi yanatakiwa kuwa ya heshima. Uvumilivu, kukimbia unapoitwa ni heshima kwa kila mwanafunzi.

Mwanafunzi unatakiwa kuwa na heshima mbele ya Bendera ya Taifa na Mbele ya viongozi.

Kusimama mistarini kwa heshima, Kugonga mlango unapoingia ofisini na kusubiri ukaribisho, kuomba radhi na msamaha unapokosea, kusalimia walimu wanapoingia darasani na nje ya darasa.

(ii) **Utii bila shuruti.** Mwanafunzi unatakiwa kutii sheria za shule, kutii walimu na wafanyakazi, kutii kengele na kukimbia kengele inapogongwa, kutii adhabu unazopewa, kutii na kuitikia wito wadharura, Kutii maelekezo ya walimu na kuyafanya kazi.

(iii) **Ushirikiano:** Unatakiwa kuonesha ushirikiano kati ya walimu na wanafunzi wenzako katika kazi za nje na masomo kwa ujumla.

(iv) **Utunzaji wa mali:** Utapaswa kutunza vifaa vyote vya shule, kutunza wa mali yako binafsi na mali za shule.

(v) **Mahudhurio:** Unatakiwa usiwe mtoro wa reje reja au wa kudumu, kutimiza wajibu wako wa darasani na nje ya darasa, kufuata ratiba ya shule kikamilifu, kuwahi shulen kila siku na kushika namba au mahudhurio ya asubuhi pamoja na kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa.

(vi) **Usafi:** Unatakiwa kuzingatia usafi wa mwili, mavazi na mazingira, kuoga kila siku kabla ya kufika shule na kufua nguo za shule.

Kumbuka mavazi ya shule si kwaajili ya kufanya kazi za shamba, kukatia majani au kufanya michezo.

(vii) **Bidii na uwajibikaji:** Unatakiwa kuonesha bidii na wajibu katika kazi za nje na katika masomo kwa kumsikiliza mwalimu darasani kwa makini, kuandika nukuu za somo, kuuliza maswali, kufanya mazoezi yote ya darasani na mittihani, kujisomea nyumbani na kushiriki mijadala (Discussions).

(viii) **Uaminifu:** Unatakiwa kuwa mwaminifu katika mambo yote ikiwemo kusema ukweli wa jambo, kutoa taarifa kwa walimu zinazo husiana na utovu wa nidhamu, kukabidhi kwa mwalimu mali uliyoiokota, kutunza mali na rasilimali za shule unapokabidhiwa.

#### 2. MAKATAZO

A. Sehemu asizoruhusiwa mwanafunzi kutemblea bila kibali maalum au ruhusa.

(i) Ofisi ya walimu (ii) Nyumba za walimu na wafanyakazi. (iii) Chumba cha kulala walimu au wafanyakazi (iv) Maabara na (v) Jikoni.

**B. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu zifuatazo.**

(i) Vilabu vya pombe (ii) Nyumba au kumbi za starehe na (iii) Nyumba za kufikia wageni

**C. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa maalumu kutoka kwa walimu.**

**3. NI MARUFUKU**

(a) Kuiba mali ya mwenzako au ya umma (b) Kufanya uasherati, ubakaji au ushoga (c) Kupiga au kupigana (d) Kuharibu mali ya umma (e) Kupata kutoa au kusababisha mimba ndani au nje ya shule (f) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au kuchafua amani au usalama wa watu  
(g) Kukataa adhabu (h) Kumiliki na kutumia simu ya mkononi (i) Kuibia mtihani au kufanya udanganyifu katika mitihani.

**4. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi, Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.  
(ii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta, biashara yamadawa yote ya kulevyta.  
(iii) Makosa mengine ya Jinai.  
(iv) Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzako au mtumishi.  
(v) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.  
(vi) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa.  
(vii) Kuoa au kuolewa.  
(viii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.  
(ix) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.  
(x) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.  
(xi) Kukataa adhabu halali.  
(xii) Utoro sugu wa shule.  
(xiii) Kuacha kufanya mazoezi na mtihani.  
(xiv) Kujiachisha shule mwenyewe.

**5. ANGALIZO:** Ni jukumu la kila mwanafunzi kufuata Sheria Taratibu na Kanuni zilizowekwa pamoja na nyingine zitakazoelekezwa ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni watekelezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi ukiwasikiliza walimu utafikia malengo yako.

Mtu hawezi kudai kuwa ameelimika wakati hana tabia inayokubalika katika jamii yake. Licha ya Elimu yake MTU HUYO NI MWONGO.

***NAKUPONGEZA SANA NA KARIBU NDURUMO SEKONDARI***